
# MWANASHERIA

JARIDA LA AFISI YA MWANASHERIA MKUU ZANZIBAR

AGC ZANZIBAR ATTORNEY-GENERALS CHAMBERS

# "HAKI NA WAJIBU"



SCAN ME

TOLEO LA 003 JANUARI - JUNI 2025

Scan kusoma Jarida kielektroniki

www.agcz.go.tz

HALIUZWI

# SALAMU ZA MHE. MWANASHERIA MKUU



**Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar ni taasisi ya umma inayoshughulika na utekelezaji wa kazi za Mwanasheria Mkuu kama zinavyoelezwa kwenye kifungu cha 56 cha Katiba ya Zanzibar ya 1984 pamoja na yanayobainishwa kwenye kifungu cha 14(1) - (4) cha Sheria ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu (Utekelezaji wa Majukumu) Nam. 6 ya 2013.**

Afisi ya Mwanasheria Mkuu katika kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, imeona kuna umuhimu wa kuanzisha JARIDA LA MWANASHERIA, ikiwa ni njia moja wapo ya kuelimisha umma juu ya shughuli zetu za kawaida.

Jarida hili ambalo hutolewa kila baada ya miezi sita, huchapisha makala pamoja na taarifa mbali mbali zitokanazo na shughuli zinazotekelezwa na Afisi yetu.

Hili ni Toleo la Tatu (003) katika mfululizo wa utoaji wa Jarida hili. Toleo hili ni kwa ajili ya kipindi cha Januari – Juni 2025.

Kwa kuwakumbusha wasomaji waliowahi kusoma matoleo yaliyotangulia ya Jarida letu, na kuwaarifu wasomaji wapya, Toleo la Kwanza (001) lilihusika na kipindi cha Januari – Juni 2024 na Toleo la Pili (002) ni kwa ajili ya kipindi cha Julai – Disemba 2024.

Tunataraji wadau wetu waliobahatika kusoma matoleo mawili yaliyopita wamefurahia matoleo hayo na kunufaika na maudhui yake.

Aidha, tunategemea kwamba wadau hao sasa wako tayari kupokea Toleo hili la tatu, ili waweze kujiongezea upeo na maarifa zaidi kuhusiana na shughuli za Afisi ya Mwanasheria Mkuu, pamoja na baadhi ya shughuli katika Sekta ya Sheria na Serikali kwa ujumla, ambazo Afisi ya Mwanasheria Mkuu ni mdau au ilihusika na utekelezaji wake katika kipindi hicho.

Napenda kueleza furaha yangu, kwa niaba ya Afisi yetu, kwa maoni mbali mbali tuliyoyapokea kutoka kwa wadau waliobahatika kusoma matoleo mawili yaliyopita.

Katika maoni hayo, wasomaji wengi wametupongeza kwa kuanzisha Jarida na kueleza kuvutiwa na maudhui ya Habari pamoja na Makala zilizohusika.

Hata hivyo, baadhi yao walitoa mapendekezo yao na walishauri baadhi ya mambo ya kuzingatia na kufanya baadhi ya marekebisho, kwa nia njema ya kutuwezesha kuimarisha Jarida letu ili matoleo yanayofuata yawe bora na yenye kuvutia zaidi.

Kwa ujumla, tunawashukuru wasomaji wetu hao na kwa unyenyekevu tunawaeleza kuwa maoni na mapende kezo yao tumeyapokea na tunayachukua kwa ajili ya kuyafanyia kazi.

Kwa muhtasari Toleo hili linajumuisha taarifa sita na makala mbili. Taarifa hizo ni Uadilifu na Mifumo Imara ya Utoaji Haki, Wito kwa Watumishi kushiriki Uchaguzi Mkuu wa 2025, Mahkama kulitupa Ombi la Kikatiba la Rashid Adiy, Uzinduzi wa Ripoti ya Udhalilishaji.

Taaifa nyengine ni Wito wa Jamii kusajili Ardhi pamoja na pongezi kwa Timu kufikia hatua ya Robo Fainali ya mashindano ya Mei Mosi. Aidha, makala mbili zilizomo katika Jarida letu ni Mchakato wa Kisheria kuhusu ugawaji wa Eka Tatu za Ardhi, na Usimamizi na Ushauri wa Mikataba ya Serikali.

Tunamshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutuwezesha kulikamisha Toleo hili. Kipekee kabisa, tunawashukuru waandaaji wote wa Habari, Makala, pamoja na taarifa mbali mbali zilizojumuishwa kwenye Toleo hili, na tunawaombea afya njema, ili waendelee kutoa mchango wao katika maandalizi ya matoleo yatakayofuata ya Jarida letu.

Pamoja na shukrani hizo, kwa moyo mkunjufu kabisa, tunawakaribisha wadau wetu waliojaaliwa kupata na kuyasoma matoleo yaliyopita ya Jarida letu, pamoja na wale ambao hawajawahi kupata fursa hiyo, watenge muda kidogo wa kusoma Toleo hili.

Matarajio yetu ni kwamba watafurahia maudhui ya Jarida letu na watatupatia maoni, ushauri na mapendekezo yao, kwa lengo la kuliimarisha na kuja na matoleo mazuri zaidi siku zijazo.

Ahadi yetu kwenu ni kuyapokea maoni, ushauri na mapendekezo yenu na kujitahidi kuandaa matoleo bora zaidi yatakayofuata.

**Dkt. Mwinyi Talib Haji,**
**Mwanasheria Mkuu,**
**Zanzibar.**

AGC ZANZIBAR ATTORNEY-GENERAL'S CHAMBERS

**Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar,**
**S.L.P. 259,**
**Mazizini, Zanzibar,**
**Tanzania.**
**Simu : + 255 22 233455**
**barua pepe:**
**agcsmz@agcz.go.tz**
**www.agcz.go.tz**

SCAN ME

# TAHARIRI



**BODI YA WAHARIRI**

**Mwenyekiti:**
Shaaban Ramadhan Abdalla
(Naibu Mwanasheria Mkuu)

**Wajumbe:**
Mdungi M. Mdungi
Salim M. Abdalla
Asya M. Ahmed
Shufaa A. Khamis
Abeid M. Saleh
Hamisa M. Mmanga
Abdulghani I. Zubeir
Faki H. Mjaka

**Msanifu:**
Kombo Zubeir (mzubeir)

**Mshauri:**
Ramadhan M. Suleiman

**Kwa mara nyengine tunakuja mbele yenu tukiwa na toleo jipya la Jarida la MWANASHERIA. Hili ni Toleo la tatu (003) katika mfululizo wa utoaji wa Jarida letu ambalo huwa linatolewa kila baada ya Miezi Sita. Tunamshukuru Mungu kwa kutuwezesha kukamilisha Toleo hili.**

Toleo hili linajumuisha Makala mbili ambazo ni Mchakato wa Ugawaji wa Eka Tatu za Ardhi Kisheria na Usimamizi na Ushauri wa Mikataba ya Serikali. Makala hizi zimejumuishwa katika toleo hili kutokana na umuhimu wake kwa Serikali na kwa jamii.

Ugawaji wa eka tatu ni muhimu kwa sababu ni miongoni mwa sera iliyotekelezwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar mara tu baada ya Mapinduzi matukufu ya mwaka 1964.

Sera hii ina athari kijamii na kiuchumi kwa watu wa Zanzibar, hasa katika wakati huu wa utekelezaji wa sera za uwekezaji wa kiuchumi na mwamko wa wananchi katika kujitafutia maendeleo ya makaazi ya kuishi.

Aidha, umuhimu wa Makala hii pia unatokana na changamoto mbali mbali zinazojitokeza katika masuala ya umiliki wa ardhi pamoja na utamaduni wa watu kujipatia ardhi na kujihalalishia matumizi ya ardhi hiyo pasipo kufuata sheria katika maeneo yote ya Zanzibar.

Kwa upande wa Makala ya Usimamizi na Ushauri wa Mikataba ya Serikali imepata nafasi katika Toleo hili kwa sababu ni miongoni mwa majukumu ya kisheria ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu.

Sababu nyengine, ni umuhimu wa mikataba hiyo kwa Serikali katika kuimarisha rasilimali za taifa na kuleta ufanisi katika usimamizi wenye viwango bora na tija kwa umma.

Pamoja na Makala hizo, Toleo hili lina taarifa sita za kihabari ambazo zinatokana na matukio mbali mbali ya utekelezaji wa shughuli za Afisi ya Mwanasheria Mkuu au taasisi nyengine za Serikali zenye mnasaba na masuala ya kisheria au utekelezaji wa shughuli nyengine za Serikali.

Taarifa hizo ni Uadilifu na Mifumo Imara ya Utoaji Haki, Wito kwa Watumishi kushiriki Uchaguzi Mkuu wa 2025, Mahkama kulitupa Ombi la Kikatiba la Rashid Adiy, Uzinduzi wa Ripoti ya Udhalilishaji, Wito wa Jamii kusajili Ardhi pamoja na Pongezi kwa Timu ya Afisi kufikia hatua ya Robo Fainali ya mashindano ya Mei Mosi.

Habari hizi zimechaguliwa kwa umuhimu wake kwa utekelezaji bora wa shughuli za nchi, utendaji wenye tija wa majukumu ya Serikali, ushiriki mzuri wa wananchi katika utoaji wa haki za kiraia, uimarishaji wa nyenzo za kutumia katika mapambano dhidi ya vitendo vya udhalilishaji na njia sahihi za kufanya kwa utambuzi wa ardhi na kupunguza migogoro ya ardhi itokanayo na matumizi ya ardhi yasiyofuata sheria.

Pamoja na makala na habari hizo, Toleo hili limepambwa na picha mbali mbali zinazohusiana na mada za jarida kwa ajili ya kusherehesha na kuonesha uhalisia wa maelezo ya mada, shairi na kibonzo kwa ajili ya kuvutia zaidi wasomaji, kuongeza uzuri na kukazia maudhui ya mada hizo.

Lengo letu katika mchanganyiko huo ni kutufanya tuweze kutimiza jukumu letu la kitaasisi la kutoa taarifa, elimu na baadhi ya mafunzo yanayohitajika kwa umma, juu ya shughuli tunazofanya katika Afisi ya Mwanasheria Mkuu, kwa kutumia Jarida hili.

Kwa ujumla, Toleo hili la Jarida la MWANASHERIA limekamilika kutokana na moyo wa kujitolea, bidii, na kazi nzuri iliyofanywa na wadau wote wanaohusika na kazi hii walioshiriki katika maandalizi yake wakiwemo waandishi wa makala na habari, mshairi, msanii wa kibonzo, Bodi ya Wahariri, Msanifu pamoja na Mshauri wa Jarida.

Kwa dhati kabisa na kwa niaba ya Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar, tunawashukuru hao wote kwa kukamilisha kazi hii kwa umahiri na umakini mkubwa. Aidha, tunawashukuru watu wote ambao hawakutajwa hapo juu, ambao kwa namna moja au nyengine wameshiriki kufanikisha kazi hii.

Ushiriki wao bila shaka una mchango mkubwa katika kuikamilisha kazi hii. Kwa ujumla, tunathamini mchango wa kila mmoja wao na kwa moyo mkunjufu, tunakaribisha ushiriki wao katika matoleo mengine yatakayofuata.

Mwisho, tunatoa shukrani za awali kwa wasomaji wa Toleo hili na tunakaribisha maoni yao kwa anwani za mawasiliano za Afisi

**Shaaban Ramadhan Abdalla,**
**Mwenyekiti wa Bodi ya Wahariri.**




*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi akihut ya Sheria Zanzibar. Hafla hiyo ilifanyika katika Uwanja wa Mahkama ya Mkoa wa Mjini Magh*

# Dkt. Mwinyi: Uadilifu, mifumo ya utoaji haki huwapa wananchi imani

**NA MWANDISHI WETU**

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi amesema, utekelezaji wa Sheria kwa uadilifu na kuwepo kwa mifumo imara ya upatikanaji wa haki ni msingi katika kujenga na kukuza imani ya wananchi kwa Serikali.

Rais Dkt. Mwinyi amesema hayo katika hafla ya kilele cha maadhimisho ya Wiki ya Sheria iliyofanyika katika uwanja wa Mahkama ya Mkoa wa Mjini Magharibi Mazizini, Wilaya ya Mjini, Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.

Amebainisha kuwa utekelezaji wa sheria kwa uadilifu, huleta amani na utulivu katika nchi pamoja na kuchochea mafanikio ya kiuchumi na maendeleo ya jamii.

Amesema, Serikali imekuwa ikisisitiza umuhimu wa Maadili kwa Watumishi wa Umma pamoja na upande wa Mahkama, kwani suala hilo lina uzito wa aina yake katika upatikanaji wa haki.

Ameeleza kuwa miongoni mwa mambo yanayodhoofisha misingi ya haki na utawala bora ni kuwepo kwa vitendo vya rushwa, uzembe, kukosa uwajibikaji na ukiukwaji wa maadili.

Halikadhalika Dkt. Mwinyi amewakumbusha watendaji wa Mahkama na wadau wake, juu ya umuhimu wa kuzingatia maadili katika utoaji wa haki kwa wananchi.

Dkt. Mwinyi amesisitiza kuwa Serikali itaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuimarisha ustawi wa jamii na kiuchumi kwa lengo la kuwawezesha wananchi hususani wa kipato cha chini kuondokana na umasikini. Hivyo, mafanikio ya Serikali katika ustawi wa jamii ni lazima yaendane na sekta ya sheria ikiwemo Mahkama.

Katika hatua nyengine, Dkt. Mwinyi amefahamisha kuwa wakati umefika kwa Mahkama kuongeza kasi ya kuwa na taratibu nyepesi za ufunguaji na utatuzi wa mashauri zitakazotilia mkazo njia mbadala za utatuzi wa migogoro katika jamii.

Awali akitoa salamu za Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar katika maadhimisho hayo, Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Dkt. Mwinyi Talib Haji amesema, Afisi hiyo inaendelea na majukumu yake ya msingi ikiwemo kuiwakilisha Serikali na Taasisi zake katika mashauri ya kesi za madai yaliopo mahkamani.

Aidha, amesema Afisi inaendelea kutoa huduma za ushauri wa




*ubia katika kilele cha Siku*
*aribi Mazizini Unguja.*

kisheria kwa wananchi wanaowasilisha malalamiko dhidi ya Serikali, sambamba na kuendelea kusimamia na kutoa ushauri juu ya mikataba inayofungwa kwa niaba ya Serikali.

Katika kuhakikisha upatikanaji wa Sheria, Mwanasheria Mkuu amesema, Afisi imechukua hatua ya kuzikusanya Sheria za Zanzibar kuanzia mwaka 1908 hadi kufikia mwaka 2024 kwa njia ya nakala laini (soft copies).

Amesema, Sheria hizo zitawekwa katika tovuti (website) ya Afisi, ambapo zitaweza kupatikana kwa njia ya mtandao na hivyo kuwawezesha wadau wote wa sheria na wananchi kwa ujumla kuzitumia sheria hizo katika shughuli zao mbali mbali.

Dkt. Mwinyi amesema, mbali na hatua hiyo ya awali, Afisi imekamilisha utayarishaji wa Mswada wa Sheria ya Mapitio na tayari mswada huo umesharidhiwa na kuidhinishwa na Baraza la Mapinduzi ukisubiri kuwasilishwa katika Baraza la Wawakilishi Zanzibar kwa hatua zinazofuata.

"Sheria mpya ya Mapitio ya Sheria itakapokamilika, itatoa uwezo kwa Afisi ya Mwanasheria Mkuu kuzifanyia mapitio na kuziunganisha sheria zilizofanyiwa marekebisho na hatimaye kuzichapa upya, hali hiyo itarahisisha sana kufanya Rejea ya Sheria (Reference) katika Mahkama zetu na vyombo vyengine vya utoaji haki hapa nchini", amesema Dkt. Mwinyi.

Akizungumza katika hafla hiyo Jaji Mkuu wa Zanzibar, Mhe. Khamis Ramadhan Abdalla, ameishukuru Serikali kwa uimarishaji na ujenzi wa miundombinu ya Mahkama nchini, hali inayowafanya watendaji wa Mahkama kufanya kazi katika mazingira bora.

Maadhimisho hayo ambayo hufanyika kila mwaka yaliambatana na uzinduzi wa Mwongozo wa Urejeshaji wa Mali kwa Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, uzinduzi wa Mwongozo wa Utoaji wa Adhabu wa mwaka 2025 na kukabidhi Ripoti ya Utendaji Kazi wa Mahkama ya mwaka 2024.



*Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar, Dkt. Mwinyi Talib Haji akihutubia katika kilele cha siku ya Sheria.*

# Watumishi tushiriki kwenye Uchaguzi Mkuu 2025 – Dkt. Haroun

**NA MWANDISHI WETU**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Mhe. Dkt. Haroun Ali Suleiman, amewataka watumishi wa umma, kushiriki kikamilifu katika zoezi la kupiga kura ili kutimiza haki yao ya kikatiba.

Dkt. Haroun ameyasema hayo alipotembelea Afisi ya Mwanasheria Mkuu, Mazizini, alipokuwa kwenye mwendelezo wa kuzitembelea taasisi zilizochini ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, sambamba na kupokea Taarifa ya Utekelezaji ya Miaka Mitano ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu.

Waziri huyo, amewataka watumishi wenye nia ya kushiriki kinyang'anyiro cha Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu katika nafasi tofauti za uongozi, kufuata taratibu za kuomba ruhusa ili kwenda kutimiza ndoto zao.

Waziri huyo amefafanua kuwa, Watumishi wa Umma kama ilivyokuwa kwa wananchi wengine, wana haki na fursa sawa za kushiriki katika uchaguzi, kwa kupiga kura au kugombea nafasi za uongozi ikiwemo Uwakilishi, Ubunge na Udiwani.

"Watumishi wenzangu nasisitiza umuhimu wa sote tukapige kura na kwa wale wenye nia ya kwenda majimboni nawaomba muombe ruhusa na ninamini mkifuata vyema taratibu viongozi wenu watawaruhusu, kwani hiyo ni haki yenu" alifahamisha Dkt. Haroun.

Akizungumza kuhusu Maadili ya Utumishi, Dkt. Haroun amewataka watumishi hao kufanya kazi kwa bidii, kuwa na nidhamu kwa viongozi pamoja na kuingia na kuondoka kazini kwa wakati.

Kwa upande wa viongozi, Mhe. Haroun amewahimiza kuwasimamia vyema Watumishi kutekeleza majukumu yao na pale watumishi watakapofanya vyema, kuna haja ya kuwapa motisha ili kuwahamasisha zaidi kufanya kazi kwa bidii.

Awali akiwasilisha Ripoti ya Utekelezaji wa Kazi na Majukumu ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar kwa kipindi cha Miaka Mitano (2020-2025) Mkurugenzi Rasilimali Watu, Utawala na Mipango, Bi. Fatma Iddi Ali kwa niaba ya Mwanasheria Mkuu amesema, Afisi kwa kushirikiana na Taasisi mbalimbali imeweza kuandaa Miswada 56 na hatimaye Miswada hiyo kupitishwa na Baraza la Wawakilishi na kuwa Sheria.

Aidha, Mkurugenzi huyo, amesema Afisi imeandaa Kanuni 58 pamoja na Matangazo mengine ya Kisheria 215 na kutangazwa katika Gazeti Rasmi la Serikali.

Kwa upande mwengine, Afisi imefanikiwa kuzikusanya Sheria zote za Zanzibar kwa mfumo wa nakala laini (soft copies) kuanzia mwaka 1909 hadi 2024 na hivi karibuni Sheria hizo zitawekwa kwenye tovuti ya Afisi ili wananchi waweze kuzipata kwa urahisi.

Kuhusu usimamizi wa mikataba, Mkurugenzi Fatma amesema, jumla ya Mikataba 3,802 ilitolewa ushauri wa Kisheria. Kati ya hiyo Mikataba 2,502 ilihusu ununuzi wa Bidhaa na Huduma, Mikataba 647 ilihusu Ujenzi, Mikataba 448 ni ya Ushauri Elekezi huku Mikataba 205 ikihusu Kodi.

Ameongeza kuwa, jumla ya Hati za Maelewano (MoUs) 692 zimetolewa ushauri katika sekta ya Elimu, Uchumi, Usafiri, Utalii, Makaazi, Afya, Ardhi, Ujenzi, Teknolojia, Kilimo, Utamaduni, Sheria, Mazingira na Fedha.

Akizungumzia Usimamizi wa Kesi Mkurugenzi Fatma amesema, Afisi iliendelea kuiwakilisha Serikali kwenye Mashauri ya Kesi za Madai na kutoa ushauri wa kisheria kuhusiana na mashauri hayo pamoja na kusikiliza malalamiko mbali mbali ya wananchi



*Mkurugenzi Rasilimali Watu, Uta Iddi Ali akiwasilisha Ripoti ya Utek Zanzibar kwa kipindi cha Miaka Mita*



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Mhe. Dkt. Haroun Ali Suleiman, akizungumza na watendaji wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu alipofanya ziara ya kutembelea Afisi hiyo.*

waliyoyawasilisha dhidi ya taasisi au watendaji wa Serikali.

Katika kipindi cha 2020 hadi 2025, kesi 75 zilifunguliwa mahakamani, ambapo kesi 21 zilisikilizwa na zilimalizika na kesi 20 Serikali ilishinda na kesi moja Serikali ilikata Rufaa. Kesi zilizosalia bado zinaendelea Mahakamani katika hatua tofauti.

Kuhusu Mapitio ya Sheria, Elimu na Utafiti, Mkurugenzi Fatma amesema, Afisi kwa Mwaka 2024-2025 ilifanya mapitio ya Sheria Saba (7) ambazo zimeweza kufanyiwa utafiti wa kina katika maeneo makhususi yaliyokusudiwa.

Kwa upande wa changamoto amesema, Afisi ya Mwanasheria Mkuu inakabiliwa na changamoto kadhaa ikiwemo upatikanaji wa fedha kwa wakati, ufinyu wa nafasi katika jengo la Afisi kutokana na kuongezeka kwa wafanyakazi baada ya Tume ya Kurekebisha Sheria kuunganishwa na Afisi ya Mwanasheria Mkuu.

Hata hivyo, Mkurugenzi Fatma amesema, kwa sasa, Afisi inaendelea na jitihada ya kutafuta eneo mbadala ili iweze kujenga jengo jengine la Afisi litakalokidhi mahitaji.



*wala na Mipango kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu, Bi. Fatma elezaji wa Kazi na Majukumu ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu no (2020-2025).*

# Ufahamu mchakato wa ugawaji wa eka tatu za ardhi



*Rais wa Kwanza wa Zanzibar Hayati Mzee Abeid Aman Karume na baadhi ya viongozi wa Serikali yake wakikagua mashamba wakati wa mchakato wa kugawa mashamba ya eka tatu kwa wananchi.*

**NA ALI ALI HASSAN**

EKA au kwa Kiswahili sanifu ekari, ni kipimo cha mraba kinachotumika kupimia eneo la ardhi ambacho ni sawa na yadi za miraba 4840. Hivyo, tunapozungumzia eka tatu maana yake ni yadi za miraba 4840 x 3 zinazofanya jumla ya yadi za mraba 14,520. Kipimo cha ukubwa wa eka tatu kilitofautiana kutokana na mazingira na utaalamu wa upimaji kwani sio zote zilikuwa ni eka tatu halisi. Kwa Unguja, wastani wa ardhi za eka tatu ilikuwa ni eka 3.7 ambapo kwa Pemba ilikuwa ni wastani wa eka 2 (Lugoe: 2011, uk. 14).

Hapa Zanzibar ukitaja neno eka, watu wanaelewa kwamba ni shamba ambalo mara baada ya Mapinduzi lilitaifishwa na Serikali na kuligawa kwa mwananchi wa kawaida. Mashamba hayo yaligaiwa kwa ekari tatu tatu kwa wananchi mbali mbali.

**Sheria ya Kutaifisha Mali Zisizohamishika Nam.8 ya 1964**

Baada ya Mapinduzi ya 1964, Serikali iliamua kuitangaza ardhi yote ya Zanzibar kuwa ni mali ya umma na kuigawa kwa wananchi kwa utaratibu wa eka tatu kwa ajili ya shughuli za kilimo. Sheria za kusimamia sera hiyo ya eka tatu zilitungwa.

Mnamo mwaka 1964, Baraza la Mapinduzi lilipitisha Sheria ya Kutaifisha Mali Zisizohamishika Nam.8 ya 1964. Kwa mujibu wa Sheria hiyo, Rais aliweza kuichukua mali ya mtu yeyote bila ya fidia iwapo kufanya hivyo ni kwa maslahi ya umma na hakutamletea ugumu wa maisha mmiliki wa mali hiyo. Hadi kufikia mwaka 1974, inakadiriwa kwamba mali zisizohamishika 1,155 kwa Unguja na 342 kwa Pemba zinazofanya jumla ya mali 1,497 zilitaifishwa na kutangazwa katika Gazeti Rasmi la Serikali. Mali hizi ni mkusanyiko wa mashamba, nyumba na viwanda. Ardhi zilizotolewa kwa matumizi ya eka tatu zilitolewa kwa wanufaika wanaofika 23,715 na



*Rais wa Kwanza wa Zanzibar Hayati Mzee Abeid Aman Karume (katikati) akiwa katika zoezi la kugawa mashamba ya eka tatu kwa wananchi mara baada ya kufanyika Mapinduzi mwaka 1964.*

zilijumuisha ukubwa wa kufikia ekari 71,145 (Torhonen: 1998, uk.34).

Kifungu muhimu katika Sheria hiyo ni kifungu cha 8(1), ambacho kilieleza kwamba uchukuaji wa mali ni lazima utangazwe katika Gazeti Rasmi la Serikali na kabla ya kutaifishwa kwa mali ilizingatiwa kuwa utaifishwaji huo bila ya fidia hautamsababishia mmiliki hali ngumu ya maisha.

Kwa kuwa mali zilizohitajika kutaifishwa zilikuwa nyingi na kwa kuwa ni Rais pekee aliyepewa mamlaka ya kutaifisha, ikalazimu mamlaka hayo kushushwa kwa Waziri yeyote. Sheria ya Kutaifisha Mali Zisizohamishika Nam.8 ya 1964 ilibidi irekebishwe kwa kupitisha Sheria ya Kutaifisha Mali Zisizohamishika (Marekebisho) Nam. 16 ya 1964, iliyompa mamlaka Waziri yeyote kusaini hati ya kutaifisha mali kwa maslahi ya umma.

**Sheria ya Ardhi ya Umma Nam. 13 ya 1965**

Mnamo mwaka 1965, Baraza la Mapinduzi lilipitisha Sheria iliyojulikana kama Sheria ya Ardhi ya Umma Nam. 13 ya 1965. Sheria hiyo yenye vifungu viwili tu ilikuja kuiweka ardhi yote ya Zanzibar inayomilikiwa kwa njia yoyote ile kuwa mikononi mwa Serikali. Pamoja na kutangazwa kwamba ardhi yote ni ya Serikali, kifungu cha 2(1) cha Sheria hiyo kinabainisha wazi kwamba hakitohusika na ardhi iliyoendelezwa.

Hii ina maana kwamba ardhi yote ni mali ya Serikali na ile iliyoendelezwa ni haki ya mtu aliyeiendeleza. Ardhi iliyoendelezwa hapa ilimaanisha ardhi iliyojengwa au zinazotumika kwa shughuli za kiufundi, madini au shughuli za kilimo. Kwa mtazamo huo, msimamo ukawa ardhi yote ya Zanzibar ni mali ya Serikali na wananchi wana haki ya matumizi

tu ya ardhi hiyo.

**Sheria ya Ardhi (Ugawaji) Nam. 5 ya 1966**

Katika mwaka 1966, ilipitishwa Sheria ya Ardhi (Ugawaji) Nam. 5 ya 1966. Sheria hiyo iliiwezesha Serikali kuiunganisha ardhi yote iliyoihodhi kwa mujibu wa Sheria ya Kutaifisha Mali Isiyohamishika ya 1964 na kumuwezesha Rais kwa kushauriana na Baraza la Mapinduzi kuigawa kwa wananchi wanyonge ambao hawakuwa na ardhi.

Hatua ya kwanza ilihusu ugawaji mashamba ambayo ulizalisha neno 'eka tatu'. Wananchi waliohitaji waligaiwa eka tatu za ardhi kwa ajili ya kilimo. Kwa mujibu wa kifungu cha 2(2) cha Sheria hiyo, ugawaji huo ulithibitishwa kwa kupewa Waraka wa Eka Tatu ambao ulisainiwa na Rais mwenyewe.

Kwa mujibu wa kifungu cha 3 cha Sheria hiyo, eka tatu hizo zilitolewa kwa mtu na mwenza wake kwa umri wao wote. Kwa utaratibu huo, akifariki mume ardhi hiyo inakuwa ya kizuka peke yake, haiingizwi katika mirathi ya marehemu.

Kizuka naye atakapofariki ardhi inaweza kutolewa kwa mmoja au zaidi ya warathi wa watu waliopewa ardhi, ikiwa ni pamoja na mtoto wa kulea (adopted child). Kwa hivyo, wale ambao wanajipa mamlaka ya kujirithisha mashamba ya eka tatu waelewe kwamba wanakinzana na sheria.

Waraka wa eka tatu uliambatana na masharti ya upewaji wa eka hizo. Masharti hayo yamo kwenye kipengele cha 4 cha Waraka huo ambao ni:

a. Mpewaji ana wajibu wa kuitumia ardhi aliyopewa, kuihifadhi na kuitunza, kutunza rutuba ya udongo kwa njia za kisasa za kilimo na ufugaji.
b. Mpewaji asiruhusu sehemu yoyote ya ardhi aliyopewa kuondolewa na mmong'onyoko, kuchoka kuzalisha au uharibifu wa aina nyengine.
c. Mpewaji atapanda na kulima mazao kama atakavyoelekezwa na Afisa aliyeidhinishwa.
d. Mpewaji hatofanya au kuruhusu kufanyika uchafuzi au uharibifu katika ardhi aliyopewa.
e. Mpewaji hatofanya wala kusababisha kufanyika jambo lolote ambalo linaweza kuwa kero au maudhi au kusababisha madhara kwa majirani.
f. Mpewaji hatoigawa, kuitoa, kuikodisha, kuiweka rehani au kuachana na umiliki wa ardhi hiyo.
g. Mpewaji atamruhusu afisa aliyeidhinishwa kuingia katika ardhi hiyo kwa ajili ya kuthibitisha kama masharti yanatekelezwa na atatii maelekezo halali atakayopewa na afisa huyo.

Kifungu cha 6 cha Sheria Nam. 5 ya 1966 kinahusu kukatishwa umiliki wa eka tatu kwa mpewaji



*Mwananchi (wa pili kulia) akipokea Hati ya matumizi ya ardhi kwa ajili ya kilimo kutoka kwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makaazi Mhe. Rahma Kassim Ali, kulia ni Katibu Mtendaji wa Kamisheni ya Ardhi Ndg. Mussa Kombo na kushoto ni Mwenyekiti wa Bodi ya Utendaji na Usimamizi wa Kamisheni ya Ardhi Zanzibar Dkt. Idrissa Muslim Hijja.*

aliyevunja sharti lolote kati ya hayo hapo juu au akishindwa kutekeleza maelekezo ya afisa aliyeidhinishwa.

Rais, kwa notisi iliyochapishwa katika Gazeti Rasmi la Serikali, anaweza kusitisha haki yoyote kuhusiana na ardhi hiyo. Mara inapotangazwa kukatishwa umiliki huo, Mpewaji atarejesha ardhi hiyo kwa Afisa aliyeidhinishwa na Mpewaji huyo hatostahiki fidia yoyote kwa uimarishaji aliofanya katika ardhi hiyo.

Katika mwaka 1969, Sheria ya Ardhi (Ugawaji) ya 1966 ilirekebishwa na Sheria Nam.1 ya 1969 kwa kuongeza kifungu kipya cha 7. Kifungu hicho kiliruhusu ugawaji ardhi kwa madhumuni ya ujenzi. Lengo la nyongeza hiyo lilikuwa ni kuwafanya Wazanzibari wawe na makaazi bora. Kwa mujibu wa kifungu kipya cha 7, Rais kwa kushauriana na Baraza la Mapinduzi aliweza kugawa ardhi kwa madhumuni ya ujenzi.

**Katiba ya Zanzibar 1984 na Urejeshwaji wa Ardhi iliyotaifishwa**

Ieleweke kwamba Katiba ya Zanzibar ya 1979 haikuwa na maelezo kuhusu haki za binadamu. Hivyo, hakuna mtu aliyeweza kudai kurejeshewa mali yake iliyotaifishwa kinyume cha Sheria kwa kutumia Katiba hiyo. Mazingira yalibadilika pale Katiba ya Zanzibar ya 1984 ilipoanza kufanya kazi. Katiba hiyo ilikuja na maelezo ya Haki za Binadamu na moja ya haki hizo ni kifungu cha 17 cha Kinga Kutokana na Kudhulumiwa Mali.

Kwa kutumia kifungu hicho cha Katiba, madai yalianza kumiminika mahakamani wananchi kudai kuchukuliwa ardhi zao kwa nguvu. Katika kushughulikia madai hayo, Mahakama ilikubali madai ambayo kuchukuliwa kwa ardhi inayodaiwa kulikiuka sheria tu.

**Hatua za Serikali Kukabiliana na Urejeshwaji wa Ardhi**

Kuwemo kwa Haki za Binadamu katika Katiba, hasa kifungu cha 17 cha Kinga Kutokana na Kudhulumiwa Mali kulichochea wananchi kudai mashamba yaliyotaifishwa kinyume cha utaratibu. Utetezi ambao Serikali iliutegemea ulikuwa:

a. Madai kupitwa na wakati: Kwa mujibu wa Sheria ya Kikomo, Sura ya 12, Kikomo cha muda wa madai kwa mali zisizohamishika ni miaka 12. Kwa hivyo, mtu ambaye amechukuliwa ardhi yake kwa zaidi ya miaka 12 anazuilika kudai haki yake hiyo.
b. Kusamehe: Kwamba mtu anaona mali yake imechukuliwa, mtu mwengine akaipanda miti ya kudumu mpaka imekuwa ya kuvuna wakati yeye amenyamaza, hapo baadaye anazuilika kudai.
c. Kifungu cha 4 cha Sheria ya Matumizi ya Ardhi (Land Tenure Act no.12 of 1992) kinazuia kurejeshwa ardhi zilizotaifishwa kinyume cha taratibu.

**Hatima ya Eka Tatu Kupitia Utambuzi wa Ardhi**

Mnamo mwaka 1990, Sheria ya Utambuzi Ardhi Nam. 8 ya 1990 (Land Adjudication Act 1990) ilipitishwa. Pamoja na mambo mengine, kifungu cha 18 cha Sheria hiyo kinaeleza kwamba wakati wa utambuzi, mtu ambaye anamiliki eka tatu atatambuliwa kwamba ni mtumiaji halali wa ardhi hiyo. Kwa msingi huo ni wazi kwamba wale wote wenye eka tatu watatambuliwa kwamba ni watumiaji ardhi na watapewa hati rasmi za utumiaji ardhi hizo.

Kifungu cha 69(1) cha Sheria ya Umiliki Ardhi ya 1992, pamoja na mambo mengine kimefuta Sheria inayohusu Ugawaji Ardhi, yaani hiyo Sheria ya Eka Tatu na pia Sheria ya Kutaifisha mali. Masuala hayo sasa yote yamo kwenye Sheria hiyo Namba 12 ya 1992 na utaratibu mpya umewekwa. Kwa mujibu wa Sheria hiyo ya Umiliki Ardhi ya 1992, kuna njia mbili tu za Serikali kutoa ardhi, ambazo ni:

a. Kupewa haki ya Matumizi ya Ardhi (Right of Occupancy); au
b. Kodi ya Serikali (Government lease).

**Kurejeshewa Ardhi Zinazodaiwa Kuchukuliwa Serikali**

Sheria ya Kikomo cha muda wa Madai (Limitation Decree, Sura ya 12 ya Sheria za Zanzibar) imeweka kikomo cha muda wa madai kwa mali isiyohamishika kuwa ni miaka 12. Sheria ya Utambuzi Ardhi (Land Adjudication Act) imeweka kanuni ya kumtambua mtumiaji kuwa ni yule aliyeikalia ardhi kwa miaka 12 bila kubughudhiwa. Mtu anaweza kuiomba Serikali impatie sehemu ya ardhi hiyo kama haki ya matumizi ya ardhi au kwa kukodishwa na Serikali kwa mujibu wa sheria, lakini sio kwamba ardhi hiyo ni yake.


***Rejea***

***Mika Torhonen, The past, present and future of land tenure in Zanzibar, RICS Research, 1998.***

***Furaha Lugoe, Land Markets in Zanzibar, Sustainable Management of Land and Environment – SMOLE II, 2011.***

# Mahkama yalitupa Ombi la Kikatiba la Rashid Adiy na wenzake

**NA MWANDISHI WETU**

MAHKAMA Kuu Zanzibar imeondosha Ombi la Kikatiba Nam.03/ 2024 na Ombi la Madai Nam. 100/2024 yaliyofunguliwa na Bw. Rashid Salum Adiy na wenzake 24 na imewazuia waombaji hao kufungua maombi mengine ya Kikatiba yenye mnasaba na maombi hayo.

Akitoa ufafanuzi wa hukumu hiyo, Wakili wa Serikali Mkuu kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar, Said Salim Said amesema, Bw. Rashid Salim Adiy na wenzake 24, mnamo Agosti 1 mwaka 2024 walifungua maombi ya Kikatiba Nam.03/2024 dhidi ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Aidha shauri hilo liliwahusisha Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar na Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, wakidaiwa kukiuka vifungu kadhaa vya Katiba ya Zanzibar ya 1984.

Wakili Said amebainisha kuwa, miongoni mwa vifungu vya Katiba vinavyodaiwa kuvunjwa ni pamoja na kifungu 1,4,5,6,9,10,11,12,21,23, 24, 25A, 26,27,28,30,31,32,33, 35,56,68,69,99A, 121,122,123, na kifungu 135.

Wakili Said amesema, Bw. Rashid na wenzake walifungua maombi mengine kadhaa Mahakamani ikijumuisha Ombi Nam. 100/2024 lililofunguliwa Novemba 11 mwaka 2024, ambapo pamoja na mambo mengine waombaji waliiomba Mahakama Kuu itoe amri ya kumzuia Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar kuendelea na shughuli zote za Tume ya Uchaguzi Zanzibar mpaka pale Ombi lao la Kikatiba Nam.03/2024 litakaposikilizwa na kutolewa uamuzi.



*Mawakili wa Serikali kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu wakibadilishana mawazo kabla ya kuingia ukumbi wa Mahkama Kuu Tunguu, kusikiliza kesi.*

Katika kusimamia usikilizwaji wa maombi yote ya Waombaji, Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar kwa niaba ya Serikali iliweka pingamizi tofauti za kisheria kupinga maombi ya waombaji kuanzia ombi lao la awali la Kikatiba Nam. 03/2024 na maombi mengine yote yaliyofunguliwa.

Amesema,

walifanya hivyo kwa kuzingatia utaratibu wa Mahkama kwamba pingamizi za awali za kisheria zinapaswa kusikilizwa mwanzo kabla ya maombi ya msingi hayajasikilizwa kama ilivyoelekezwa na Mahkama ya Rufani ya Tanzania.

Wakili Said amesema, katika Shauri hilo, ilikuwa ni desturi ya waombaji mara tu wanapopatiwa nakala za pingamizi za awali za kisheria zilizoibuliwa na Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar walikuwa wanaomba kuondosha maombi yao Mahkamani kabla ya kuanza kusikilizwa kwa pingamizi hizo za kisheria.

Wakili Said ameongeza kuwa, baadhi ya wakati Mahkama Kuu yenyewe ikiyaondoa baadhi maombi yao kwa kuwa yamefunguliwa kinyume na taratibu za kisheria.

Mnamo Novemba 18 mwaka 2024, Mheshmiwa Jaji wa Mahkama Kuu Zanzibar, Mhe. Said Hassan Said aliyaondoa Maombi ya Madai Nam. 79/2024 yaliyomtaka Spika wa Baraza la Wawakilishi kusimamisha mchakato wa kujadili Sheria yoyote inayolenga kufanya marekebisho ya Kifungu chochote cha Katiba ya Zanzibar mpaka pale ombi lao la Kikatiba Nam.03/2024 litakaposikilizwa na kutolewa uamuzi.

Amesema, mnamo Februari 27 mwaka 2025, waombaji kwa mara nyengine baada ya kupokea nakla za pingamizi za awali za kisheria zilizoibuliwa na Afisi ya Mwanasheria Mkuu, waliomba kuondosha maombi yao yote ya Kikatiba yaliyopo Mahakamani ikijumuisha Ombi lao la awali Nam.03/2024 ambalo ndio ombi tegemezi kwa maombi mengine yote yaliyofunguliwa baadae.

Aidha waliomba kuondoa ombi la Madai Namba 100/2024 ambalo lililenga kumzuia Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar kutokufanya shughuli yoyote mpaka pale Ombi Nam.03/2024 litakaposikilizwa na kutolewa uamuzi.

Baada ya Mahkama kuzingatia hoja ya pande zote mbili na kwa kuzingatia matakwa ya sheria yaliyoelezwa, Mahkama Kuu ilikubali ombi la Waombaji kuondosha Ombi la Kikatiba Nam.03/2024 na Ombi la Madai Namba 100/2024 kwa sharti kwamba waombaji hawatoruhusiwa kufungua tena Mahakamani maombi yenye mnasaba na maombi yao ya awali yaliyoondolewa Mahakamani.

Katika hatua nyengine Mawakili wa Serikali kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar waliiomba Mahkama iwatoze waombaji gharama za kesi na usumbufu, ombi ambalo lilikataliwa na Mahkama.



*Mawakili wa Serikali kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar wakiwa nje ya Jengo la Mahkama Kuu Tunguu mara baada ya kutoka kusikiliza kesi.*

# MATUKIO KA



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Mhe. Dkt. Haroun Ali Suleiman, (wa pili kushoto) akipata maelezo kutoka kwa Wakili wa Serikali Ndg. Yakoub Rajab Juma baada ya kutembelea Banda la Afisi ya Mwanasheria Mkuu katika Maonesho ya Wiki ya Sheria yaliyofanyika Mapinduzi Square, Kisonge Unguja. Kushoto ni Jaji Mkuu wa Zanzibar Mhe. Khamis Ramadhan Abdalla.*



*Maafisa kutoka Afisi ya Mwanashe*
*Abdulsalaami (wa tano na wa sita kulia*
*ya pamoja na washiriki wa Mafunz*
*yaliyofanyika Shanghai, China.*



*Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar, Dkt. Mwinyi Talib Haji (kushoto) akimuonesha aliyekuwa Rais wa Mahkama ya Kimataifa ya Haki (ICJ) Jaji Abdulqawi Ahmed Yusuf moja ya Kitabu cha Sheria kinachopatikana Maktaba ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu alipofanya ziara katika Afisi hiyo.*



*Naibu Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar,*
*Sadaka kwa Mlezi wa Kituo cha Watoto*
*Afisi ya Mwanasheria Mkuu Mazizini.*




*Naibu Mwanasheria Mkuu Zanzibar, Ndg. Shaaban R. Abdalla (wapili kulia) akiwa na Wafanyakazi wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu, Pemba alipotembelea kwenye Maonesho ya Kimataifa ya Biashara yaliyofanyika Viwanja vya Chamanangwe, Pemba.*



*Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Waislam*
*picha ya pamoja na Watendaji wa Afis*
*kujifunza mambo mbali mbali.*

# ATIKA PICHA




ria Mkuu Zanzibar, Salama Rama Aman na Rukia waliosimama mstari wa kwanza) wakiwa katika picha o ya Uchumi wa Pamoja na Maendeleo endelevu



*Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar, Dkt. Mwinyi Talib Haji akiwalisha keki watoto yatima wa kituo cha Mazizini Zanzibar katika hafla ya Iftari iliyoandaliwa na Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar na kuwashirikisha watoto hao.*



Ndg. Shaaban Ramadhan Abdalla (kushoto) akikabidhi Yatima cha Mazizini, Zanzibar katika hafla iliyofanyika



*Mwenyekiti wa Kamati Maalum ya Mfuko wa Ufiwa na Maafa wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar Bi Hamisa Mmanga akitoa ufafanuzi wa masuala mbali mbali ya kuimarisha mfuko huo kwa Watumishi wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu.*



m Morogoro (MUM), wanaosoma Sheria wakiwa katika i ya Mwanasheria Mkuu, baada ya kufika Afisini hapo



*Sheha wa Ukongoroni, Hassan Makame Haji akiwakaribisha Watendaji kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar kwa ajili ya kutoa elimu ya kisheria kwa umma.*

# Ripoti ya Ukatili wa Kijinsia yazinduliwa



*Naibu Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar, Ndg. Shaaban Ramadhan Abdalla (katikati) akizindua Ripoti ya Ukatili wa Kijinsia. Kulia ni Mratibu wa Mradi wa Kutokomeza Ukatili wa Kijinsia Zanzibar kutoka (UN Women) Lucy Tesha na kushoto ni Mkurugenzi Idara ya Mapitio na Utafiti wa Sheria kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu Dkt. Abdul-Nasser Hamed Hikmany. Hafla hiyo ilifanyika Ukumbi wa Maji House, Mwembe Madema, Zanzibar.*

**NA MWANDISHI WETU**

AFISI ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar imezindua Ripoti ya Ukatili wa Kijinsia ikiwa ni sehemu ya juhudi za kuundwa kwa sheria kamili inayoshughulikia tatizo hilo nchini.

Akizungumza katika uzinduzi wa ripoti hiyo uliofanyika kwenye ukumbi wa Maji House, mjini Unguja, Naibu Mwanasheria Mkuu Zanzibar, Ndg. Shaaban Ramadhan Abdalla, amesema kuna umuhimu wa kuwa na sheria mahsusi itakayosimamia vitendo vya udhalilishaji ili lengo la Serikali la kumaliza vitendo hivyo nchini liweze kutimia.

Ameongeza kuwa kutokuwepo kwa Sheria zinazohusiana na ukatili wa kijinsia kumejitokeza mapungufu ambayo yanahitaji kushughulikiwa ili kukabiliana na changamoto zinazojitokeza katika kudhibiti vitendo hivyo.

Naibu Mwanasheria Mkuu amefahamisha kuwa, uzinduzi wa utafiti huo ni hatua moja ya kuelekea kuwa na sheria inayoendana na mapambano ya vitendo vya ukatili wa kijinsia.

"Vitendo hivi vimeshamiri na kiukweli vinaumiza hivyo hatua hii sasa itatufikisha kupata sheria inayokidhi mahitaji", alisema Naibu Shaaban.

Amesema kupatikana kwa ripoti hiyo kutatoa fursa ya kuendelea na hatua nyengine hadi kupatikana kwa sheria kamili.

Akizungumzia kuhusu ripoti hiyo, Wakili wa Serikali Mkuu kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu Dk. Mahfoudha Massoud Ali, amesema Ripoti hiyo ina mapendekezo muhimu ikiwa ni pamoja na kuanzishwa kwa sheria maalum ya kusimamia masuala ya ukatili wa kijinsia.

Aidha, amesema Ripoti imependekeza utaratibu wa ufunguaji wa mashauri, haki za waathirika, msaada wa kisheria, na uanzishwaji wa nyumba salama kwa waathirika pamoja na kulinda watoa taarifa juu ya vitendo vya ukatili wa kijinsia.

Sambamba na hayo amesema Ripoti hiyo inapendekeza kuanzishwa Mfuko wa Kupambana na Ukatili wa Kijinsia na kuwasaidia waathirika wa vitendo hivyo pamoja na kuanzishwa Kituo Jumuishi (One Stop Center) ambacho kitahusisha wadau muhimu wa haki jinai.

"Tunapendekeza kuanzishwa chombo maalum cha udhibiti sambamba na kuanzishwa Kituo Jumuishi (One Stop Center) kitakachohusisha wadau muhimu wa masuala hayo ambao watashirikiana katika mapambano dhidi ya ukatili wa kijinsia", amesema Dk. Mahfoudha.

Naye Mratibu wa Mradi wa Kutokomeza Ukatili wa Kijinsia Zanzibar kutoka Shirika



***Naibu Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar, Ndg. Shaaban Ramadhan Abdalla (kulia), akimkabidhi Ripoti ya Ukatili wa Kijinsia Ndg. Fatma Serembe Khamis kutoka Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Zanzibar katika hafla uzinduzi wa Ripoti ya Ukatili wa Kijinsia iliyofanyika Ukumbi wa Maji House, Mwembe Madema, Zanzibar.***

la Umoja wa Mataifa UN Women, Lucy Tesha ameeleza kuwa, ukatili wa kijinsia ni tatizo kubwa linalohitaji usimamizi maalum, na kwamba Shirika hilo litaendelea kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuhakikisha mapambano dhidi ya ukatili wa kijinsia yanafanikiwa.

Ameeleza kuwa, Ripoti hiyo itatoa mwongozo katika kuboresha mifumo ya kisheria na kiutendaji katika kupambana na ukatili wa kijinsia.

Aidha alisisitiza kwamba hatua hizo zitasaidia kutoa msaada wa haraka kwa waathirika na kuhakikisha haki inapatikana kwa wote.

Bi Lucy aliipongeza Afisi ya Mwanasheria Mkuu kwa utafiti huo unaolenga kutoa mapendekezo ya kisheria na kiutendaji yatakayosaidia kutatua changamoto kwa lengo la kuboresha mifumo ya kisheria iliopo.

Ripoti hiyo, ambayo utafiti wake ulianza kufanyika mwishoni mwa mwaka 2023, imefadhiliwa na Shirika la Kimataifa la UN Women na inalenga kubainisha changamoto zinazokabili mfumo wa kisheria na kutoa mapendekezo ya kuboresha udhibiti wa ukatili wa kijinsia nchini.




***Naibu Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar, Ndg. Shaaban Ramadhan Abdalla (kulia) akimkabidhi Ripoti ya Ukatili wa Kijinsia Mkurugenzi Mipango Sera na Utafiti wa Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Ndg. Said Khamis Salim katika hafla iliyofanyika Ukumbi wa Maji House, Mwembe Madema, Zanzibar.***

# Fahamu Usimamizi na Ushauri wa Mikataba

NA HAMISA MMANGA

KWA mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, Mwanasheria Mkuu ndiye Mshauri Mkuu wa masuala ya Sheria kwa Zanzibar. Katika kufanya kazi zake, Mwanasheria Mkuu anatekeleza majukumu ya kuishauri Serikali kwa mujibu wa Sheria ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu (Utekelezaji wa Majukumu) namba 6 ya 2013.

Sheria hiyo imempa uwezo wa kuishauri Serikali na kusimamia mikataba yote ambayo Serikali ni sehemu ya mikataba hiyo, kusimamia kesi za madai kwa niaba ya Serikali, kuandaa miswada ya Sheria na kufanya mambo mengine yanayohusiana na masuala ya sheria kwa Zanzibar.

Kihistoria, kabla ya kutungwa kwa Sheria ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu mwaka 2013, kazi ya kutoa ushauri na usimamizi wa mikataba ilikuwa ikifanywa kwa mujibu kwa sheria zinazohusiana na manunuzi pekee ikiwa ni pamoja na Sheria ya Bodi ya Zabuni namba 5 ya 2002, Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma namba 2 ya 2005 na Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma namba 11 ya 2016. Sheria zote hizo ziliweka sharti la mkataba kupata uthibitisho kwa Mwanasheria Mkuu kabla ya kuwekwa saini na pande zote za mkataba.

Aidha, baada ya Serikali kufanya marekebisho mbalimbali kulingana na mahitaji yanayokwenda sambasamba na mabadiliko ya kiuchumi, Sheria ya Ununuzi Umma nambari 2/2025 ilitungwa na ndio inayotumika hivi sasa ambayo nayo imeendelea kuweka sharti hilo.

**AINA ZA MIKATABA KULINGANA NA MAHITAJI YA SERIKALI**

Kwa kawaida Serikali ina mahitaji yake ya kawaida kama mtu binafsi katika kupata huduma kutoka kwa watu binafsi au kampuni.

Mahitaji hayo yanaweza kuwa ni kuendeleza miundombinu kama barabara, ujenzi wa hospitali, vituo vya afya, upatikanaji wa dawa na vifaa tiba, vifaa vya maofisini na huduma nyengine.

Hivyo katika kuhakikisha mahitaji kama ujenzi, vifaa na mahitaji mengine yanapatikana, taasisi za umma zinapaswa kufanya manunuzi kwa utaratibu uliowekwa katika Sheria inayohusiana na manunuzi.

Hivyo, Sheria hiyo ya namba 2 ya mwaka 2025 imeainisha aina za mikataba kama ifuatavyo:

a. Mikataba ya ununuzi wa bidhaa (goods) mfano ununuzi wa gari na vifaa ya ofisini, kama vile kompyuta na kadhalika;
b. Mikabata ya ujenzi (works) mfano ujenzi wa miundombinu ya barabara, ujenzi wa nyumba na majengo ya ofisi na kadhalika;
c. Mikataba ya ushauri elekezi (Consultancy), mfano usanifu wa ofisi, kutoa mafunzo ya kitaalamu na




*Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar Mhe. Hemed Suleima ya kufanya kazi kwa kushirikiana kati ya Taasisi ya wasanifu Warka Water kwenye Mkutano wa Pili wa Taasisi ya (IAESZ) u*

usimamizi wa miradi na kadhalika, na

d. Mikataba isiyokua ya ushauri elekezi (Non consultancy services) mfano huduma ya ulinzi, chakula, usafi na mengineyo.

Mikataba mengine ambayo Serikali inaingia kwa malengo mahsusi ni kama ifuatavyo:

a. Mikataba ya uchimbaji na utafutaji (Exploration and Production) wa mafuta na gesi asilia;
b. Mikataba ya Ubia (Joint Venture Agreement) ambayo inahusiana na ushirikishaji wa Taasisi za Umma na sekta binafsi;
c. Mikataba ya Hati za Maelewano (Memorandum of Understanding-MoU) ambayo ni makubaliano ya kirafiki baina ya Serikali na taasisi ama za Serikali au Zisizo za Serikali au baina ya nchi na nchi;
d. Mikataba ya Ukodishaji (Lease Agreements) mfano ukodishaji wa ardhi kwa uwekezaji, ukodishaji wa nyumba au majengo ya ofisi na mashamba;
e. Mikataba ya Kimataifa ya Uwekezaji (Bilateral Investment Treaty) ambayo ni mikataba baina ya nchi na nchi kwa ajili ya kukuza na kulinda uwekezaji mfano Mkataba wa uwekezaji, mfano baina ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Canada.
f. Mikataba ya Mikopo na Ruzuku (Loans and Concession Agreement) ni aina ya mikataba ambayo serikali ama inakopa fedha au kupokea ruzuku kutoka mataifa ama mashirika ya Kikanda na kimataifa kama African Development Bank (AfDB)na Benki ya Dunia (World Bank).




*...n Abdulla akishuhudia utiaji wa saini wa Hati ya Makubaliano ...u, wahandisi na wakadiriaji majengo Zanzibar na Taasisi ya ...liofanyika katika Ukumbi wa Hotel Verde Zanzibar.*

**AINA ZA MIKATABA KWA MUJIBU WA SHERIA**

Kwa mujibu wa Sheria ya Ununuzi wa Umma Namba 2 ya 2025 imeainisha aina tofauti za mikataba ambayo Serikali inaingia. Kifungu cha 78 cha Sheria hiyo kimeainisha aina za mikataba kama ifuatavyo:

1. Mikataba ya malipo ya gharama zote kwa pamoja (Lump sum Contract);
2. Mkataba wa malipo ya Muda Maalum (Time based Contract);
3. Mkataba Endelevu (Frame-work Contract);
4. Mkataba wa Asilimia (Percentage Based Contract);
5. Mkataba wa Kurejesha Gharama (Cost Reimbursable Contract);
6. Mkataba wa Bei Maalum (Target Price Contract);
7. Mkataba wa Kipimo cha Kazi (Admeasurement Contract);
8. Mkataba wa Kudhibiti (Retainer Contract);
9. Mkataba wa Malipo ya Mafanikio (Success Fee Contract) na
10. Aina nyengine yoyote ya mikataba itakayoidhinishwa na Mamlaka

**MIKATABA YA THAMANI GANI INAWASILISHWA KWA MWANASHERIA KWA AJILI YA USHAURI?**

Kama tulivyoainisha aina za mikataba ambayo Sheria imebainisha, Sheria hiyo imeweka thamani na kiwango

maalum ambacho Mwanasheria Mkuu ataipitia na kuithibitisha.

Kabla ya kutungwa kwa Sheria namba 2 ya 2025, Sheria ya Manunuzi ya 2016 iliweka viwango mbalimbali vya thamani ya mikataba ya ujenzi, bidhaa au ushauri elekezi ambayo inapaswa kupelekwa kwa Mwanasheria Mkuu kwa ushauri na kuthibitishwa.

Jadweli la Tano la Sheria hiyo imeweka gharama ya zaidi ya shilingi milioni 15 ya mkataba wa ununuzi wa bidhaa, zaidi ya milioni 20 ya ujenzi na ushauri elekezi thamani ya mkataba ni zaidi ya milioni 5.

Kwa sasa Sheria mpya ya Ununuzi wa Umma ya 2025 imeongeza thamani ya gharama na viwango vya mkataba ili kupunguza mrundikano wa mikataba inayowasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu.

Sheria imeainisha viwango mbalimbali vya thamani ya mikataba inayopaswa kuwasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu kwa ushauri.

Kwa mujibu wa kifungu cha 74(7) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma ya 2025 imeeleza kama ifuatavyo:

"Mkataba wowote unaozidi ukomo wa thamani ndogo ya thamani ya bei ya ununuzi iliyoainishwa katika Jadweli la Tatu la Sheria utahakikiwa na Mwanasheria Mkuu kabla ya kusainiwa na wahusika".

Aidha Jadweli la Tatu la Sheria limeweka ukomo wa thamani ya bei ya mkataba ambayo Mwanasheria Mkuu ataihakiki na kuidhinisha kwa ajili ya kuendelea na hatua za kusaini na kuanza kazi kwa mkataba husika. Aina za viwango vilivyoainishwa ni kama vifuatavyo:

a. Kwa mikataba ya bidhaa (Goods): thamani ya mikataba hiyo ni zaidi ya Shilingi Milioni 150 na kuendelea;
b. Kwa mikataba ya Ujenzi (Works): thamani ya mikataba hiyo ni Zaidi ya Shilingi Milioni 300 na kuendelea na
c. Kwa mikataba ya Ushauri Elekezi: thamani ya mikataba hiyo ni Zaidi ya Shilingi Milioni 60 na kuendelea.

Hivyo, mikataba yote chini ya kiwango cha thamani kilichoainishwa hapo juu kwa mujibu wa kifungu cha 74(8) itahakikiwa na Afisa Sheria au Wakili wa Serikali wa Taasisi Nunuzi husika kabla ya kusainiwa.

**MAMBO YA KUZINGATIA KATIKA KUTOA USHAURI WA KISHERIA**

***1. Kulinda maslahi ya Serikali***

Kama tulivyoeleza hapo juu Mwanasheria Mkuu ndiye Mshauri Mkuu katika masuala yote ya kisheria kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Miongoni mwa maadili ya uanasheria ni kufanya kazi na kulinda maslahi ya mteja kwa kiwango cha juu.

Hivyo, Mwanasheria Mkuu katika kutekeleza kazi yake na kufuata maadili ya taalum ya Sheria anapopitia mikataba anaangalia kwa kiasi kikubwa maslahi ya Serikali katika maeneo matatu ama kushauri baadhi ya vipengele vibadilishwe au kubadilisha dhana ya mradi unaotegemewa kufunga mkataba au kushauri kutofunga mkataba husika.

***2. Kuangalia thamani halisi ya fedha (Value for Money)***

Kwa bidhaa, ujenzi au huduma: Kwamba Mwanasheria Mkuu katika kufanya kazi yake ya kutoa ushauri wa kisheria katika mikataba anazingatia thamani halisi ya fedha ya ununuzi na



*Mradi wa Nyum... Serikali ya Mapindu...*

bidhaa, ujenzi au huduma zinazotaka kutolewa au huduma inayotarajiwa kupatiwa.

Mwanasheria Mkuu anaoanisha thamani kwa maslahi mapana ya nchi na kuangaliwa tija kwa kile kinachotarajiwa kupatikana.

***3 Kuangalia na kuoanisha masharti ya mkataba na masharti ya sheria (Compliance of the provisions of the law):***

Katika kutekeleza kazi ya ushauri katika mikataba, kwa kawaida Mwanasheria Mkuu hupitia mikataba inayowasilishwa na kupitia masharti ya Sheria ziliopo na kutoa ushauri wa kisheria unaofaa.

Iwapo itaonekana kwamba masharti ya mkataba yapo



...ba za kisasa zilizopo Mombasa, Zanzibar ambazo ni matokeo ya Mikataba yenye tija inayosainiwa na ...uzi ya Zanzibar.

kinyume na masharti ya Sheria, Mwanasheria Mkuu ataelekeza kuondoshwa kwa vifungu vinavyokiuka mkataba na badala yake kuelekeza viwekwe vifungu vyengine kwa mujibu wa sheria.

**Changamoto katika usimamizi wa mikataba**

Katika usimamizi wa mikataba, Afisi inakabiliwa na changamoto mbali mbali ikiwa ni pamoja na uhaba wa watendaji wenye uwezo na taaluma mahsusi zinazoendana na miradi ya kimkakati ya Serikali ya Awamu ya Nane. Hali hii inapelekea mahitaji ya mafunzo ya mara kwa mara kwa ajili ya kuwaongeza ujuzi na uzoefu wa taaluma mahsusi kama za mafuta na gesi, uchumi wa buluu na fani nyengine zinazowiana na miradi ya kimkakati.

Mbali na changamoto za ndani katika usimamizi wa mikataba, Afisi ya Mwanasheria Mkuu nayo inapitia katika changamoto mbalimbali kufuatia Rasimu za mikataba mbalimbali zinazowasilishwa. Rasimu hizo wakati mwengine zinakosa kuambatanishwa na vielelezo muhimu, kwa mfano, katika mkataba wa Mshauri Elekezi inashindwa kuambatanisha na Hadidu Rejea au hati nyengine zinazohusika moja kwa moja na mkataba husika.

Aidha, Afisi inaweza kupokea Rasimu ya Mkataba wa Nyongeza ambao unalenga kufanya marekebisho ukiwa mkataba huo umemaliza muda wake. Wakati mwengine rasimu ya mkataba inawasilishwa nje ya muda unaopaswa kuwasilishwa kwa mujibu wa Mpango wa Manunuzi kitendo ambacho kinapelekea kuharakishwa na kutoa ushauri chini ya kiwango.

Kutokana na changatoto zilizoainishwa hapo juu, ni vyema kuwajengea uwezo watendaji katika fani mahsusi ili kuongeza ufanisi na kuleta tija katika kutoa ushauri na usimamizi wa mikataba.

Kwa Taasisi mbali mbali zinazoleta Mikataba katika Afisi ya Mwanasheria Mkuu ni vyema kufuata mpango wa manunuzi ili mchakato wa kufunga mkataba uwe na tija na maslahi bora kwa umma pamoja na kufuata sheria, kanuni na miongozo.



*Fadhil Said Mlenge mkaazi wa Ukongoroni akitoa maoni yake katika mkutano wa kuwajengea uwezo wananchi kuhusu masuala ya kisheria uliofanyika huko Ukongoroni Mkoa wa Kusini Unguja.*

# Wakili atoa wito kwa jamii kusajili Ardhi zao

**NA MWANADISHI WETU**

WAKILI wa Serikali Mkuu kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar, Hamisa Mmanga, amewataka wananchi kusajili ardhi zao na kupata Hati za umiliki kwa mujibu wa Sheria ya Umiliki Ardhi Nambari 12 ya mwaka 1992.

Amesema kufanya hivyo ni miongoni mwa njia zitakazosaidia kutambulika vyema ardhi zao na kupunguza migogoro inayoibuka kwenye maeneo mengi ya Unguja na Pemba.

Wakili Hamisa ameyasema hayo kwa nyakati tofauti alipokuwa akiwasilisha mada kuhusu taratibu sahihi za umiliki wa ardhi katika Shehia ya Mahonda Mkoa wa Kaskazini Unguja na Shehia ya Ukongoroni, Mkoa wa Kusini Unguja ikiwa ni mwendelezo wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu kutoa elimu ya kisheria kwa wananchi.

Aidha amewaomba wananchi hao wakati wa kuweka na kuandika mipaka ya ardhi, kueleza urefu na upana wa eneo la umiliki badala ya kuandika tu upande fulani Ardhi imepakana na nani.

"Haitoshi tu kuandika katika nyaraka kuwa upande fulani umepaka na nani na upande fulani umepakana na nani, kuna haja ya kuelezea pia upana na urefu wa eneo husika", alisema Wakili Hamisa.

Wakitoa maoni katika mikutano hiyo, wananchi hao wameiomba Serikali kuweka fomu za uhaulishaji wa Ardhi kwenye ofisi za Masheha ili kuwaondoshea usumbufu wa kuzifuata fomu hizo mbali na maeneo yao.

Kuhusu masuala ya udhalilishaji, wananchi hao wameiomba Serikali kuangalia upya adhabu ya makosa ya udhalilishaji, ili kuwatia hatiani kwa pamoja wanawake na wanaume wanaofanya makosa hayo badala ya hivi sasa kutiwa hatiani wanaume pekee.

Haji Fadhil Mkadamu mkaazi wa



*Wakili wa Serikali Mkuu kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar, Hamisa Mmanga akiwasilisha mada kuhusu utaratibu wa umiliki wa ardhi katika Shehia ya Mahonda Mkoa wa Kaskazini Unguja.*

Mahonda amedai kuwa, kwa sasa waathirika wakubwa ni wanaume hata ikiwa waanzilishaji wa kosa hilo ni wanawake, hivyo amesema ipo haja ya hali hiyo kubadilishwa.

"Wanasheria tunaomba ufafanuzi, mwari anaweza kutoka Nungwi mwenyewe kuja kumfuata mwanamme Ukongoroni wazazi wao wakijua na kesi ikaendeshwa, ni mwanamme pekee atakayetiwa hatiani", alihoji Haji Fadhil Mkadamu.

Naye Fadhil Said Mlenge mkaazi wa Ukongoroni, amesema kwa hali inavyoenda idadi ya vijana wa kiume itaendelea kujaa kwenye Vyuo vya Mafunzo kutokana na kutiwa hatiani huku baadhi ya wanawake ambao ni chanzo cha makosa hayo wakiwa uraiani wakiendelea kuwafungisha wanaume.

Aidha ameomba Afisi ya Mwanasheria Mkuu kuendelea kutoa elimu ya sheria ili jamii iendelee kupata uelewa badala ya kusubiri kutoa elimu hiyo kila ifikapo wiki ya sheria.

Akijibu hoja za wananchi hao, Wakili wa Serikali Mkuu kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar, Mbarouk Othman amesema Afisi imesikia malalamiko hayo ya wananchi na itatafuta namna ya kuyashughulikia malalamiko hayo.

Wakili Mbarouk amesema kosa la ubakaji linaweza kumtia hatiani mtu yeyote bila kujalisha umri, hivyo jambo la muhimu ni kwa vijana na wazee kujiepusha kutenda kosa hilo ambalo halina dhamana.

Wakili Mbarouk amesema Afisi ya Mwanasheria Mkuu itaendelea kutoa elimu kwa wananchi wa Unguja na Pemba kupitia Shehia zao ili kuhakikisha wanakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu Sheria ili waepuke kuzivunja sheria.

Katika mikutano hiyo Afisi ya Mwanasheria Mkuu iliwasilisha mada tatu ambazo ni Haki za Binadamu iliyowasilishwa na Wakili Sumaiya Hassan Awadh, Taratibu sahihi za umiliki wa Ardhi iliyowasilishwa na Wakili wa Serikali Mkuu Hamisa Mmanga na mada ya namna ya kuishitaki Serikali iliyowasilishwa na Wakili wa Serikali Mkuu Mbarouk Othman.

# Kibonzo..


NENDA KAWAMBIE WANAOTAKA KUTANGAZA NIA, MWENYE JIMBO NIPO. SHAURI YAO!
MBONA UNA WATISHA WAKATI KUGOMBEA NI HAKI YAO YA KIKATIBA.

# Nasaha za Mshairi

## SHAIRI: MWAKA WA UCHAGUZI NA HAMAD ALI KOMBO (DKT. MSHIKO)

**1**
Yarabi mola Rabuka    Peke tunokuamini
Kwa haja ndo mwafaka    Akhera na duniani
Mwaka uno umefika    Uchaguzi wa nchini
Ni mwaka wa uchaguzi    Idumu yetu amani

**2**
Mola wetu muhibaka    Twakuomba ya manani
Mwezi wa kumi ikifika    Mwana hatumwi dukani
Uchaguzi utafika    Bara pamwe visiwani
Ni mwaka wa uchaguzi    Idumu yetu amani

**3**
Afisi inatutaka    Sheria tufuateni
Za Nchi zilizowekwa    Zisijevunjwa jamani
Uchaguzi ukifika    Vurugu tusifanyeni
Ni mwaka wa uchaguzi    Idumu yetu Amani

**4**
Ofisi mwanasheria    Twaomba zingatieni
Zifatwe zote sheria    Zisipindishwe pembeni
Alo juu ya sheria    Hayuko hilo juweni
Ni mwaka wa uchaguzi    Idumu yetu amani

**5**
Nchi inayosheria    Na nyingi zake kanuni
Pia demokrasia    Ipo hapa Tanzani
Hupingwi wakuchagua    Chagua uno amini
Ni mwaka wa uchaguzi    Idumu yetu amani

**6**
Kupiga na kupigiwa    Ni haki yako amini
Sio kwendachaguliwa    Kachaguwe wewe kwani
Yule unayetambua    Ndio lako tumaini
Ni mwaka wa uchaguzi    Idumu yetu amani

**7**
Hakiyo sipotumia    Utamlaumu nani
Fika haraka tambua    Pale kwako kituoni
Kura unapopigia    Fujo iweke pembeni
Ni mwaka wa uchaguzi    Idumu yetu amani

**8**
Kura kishajipigia    Ondoka nenda nyumbani
Jukumu lilobakia    Ni la Tume ya nchini
Haki yako utapewa    Haibezwi asilani
Ni mwaka wa uchaguzi    Idumu yetu amani

**9**
Wito pia nnatoa    kwa vijana wa nchini
Sheria kutochukua    ya kukiuka kanuni
Hatua itachukua    ya kuwekwa mtu ndani
Ni mwaka wa uchaguzi    Idumu yetu Amani

**10**
Kachague unotaka    Wataoshika sukani
Watakaochakarika    Sio kukaa vitini
Uchochezi wasotaka    Na watu kuwafitini
Ni mwaka wa uchaguzi    Idumu yetu amani

**11**
Sote tutambuwe fika    Dhima iwa mikononi
Uchaguzi tunataka    Wa salama na Amani
Mwenyezi zako baraka    Tupe sije tafrani
Ni mwaka wa uchaguzi    Idumu yetu amani

**12**
Amani ikichafuka    Takuwa kitahanani
Uchaguzi tachafuka    Fimbo mpaka kichwani
Yatazuka yakuzuka    Uhasama majirani
Ni mwaka wa uchaguzi    Idumu yetu amani

**13**
Natuikate haraka    Mizizi ya wafitini
Isimee ikafika    Ikaleta uhaini
Tulale bila mashaka    Vyema mwetu majumbani
Ni mwaka wa uchaguzi    Idumu yetu amani

**14**
Dua tunaipeleka    Kwako ilahi manani
Ilinde nayo gharika    Nchi yetu Tanzani
Isije kutetereka    ikaingia mashakani
Ni mwaka wa uchaguzi    Idumu yetu amani



*Kikosi cha Timu ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu kilichofi*

# Timu ya Mwanasheria Mkuu yapongez

**NA MWANDISHI WETU**

NAIBU Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar, Ndg. Shaaban Ramadhan Abdalla, ameipongeza timu ya soka ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu, kwa kufikia hatua ya robo fainali kwenye michuano ya Mei Mosi mwaka huu.

Naibu Mwanasheria Mkuu alitoa pongezi hizo katika mahojiano na Mwandishi wa habari hizi ambapo amesema, ameridhishwa na kiwango kikubwa cha soka kilichooneshwa na timu hiyo hasa ikizingatiwa kuwa ni mara ya kwanza kushiriki mashindano hayo.

Naibu huyo amesema amelipa jukumu dawati la ufundi la timu hiyo kuhakikisha inajiandaa vyema kwa lengo la kuongeza kiwango ili kwenye mashindano ya mwakani dhamira iwe ni kuchukua ubingwa.

Alitumia fursa hiyo kuwahakikishia wachezaji na dawati la ufundi la timu hiyo kwamba Afisi itaendelea kuwapatia ushirikiano wa kutosha ili kutimiza lengo hilo.

Kwa upande wa Nahodha wa Timu ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu, Ndg. Farid Salum Maulid, amesema kilichowaangusha kiasi cha kushindwa kuchukua ubingwa ni kukosa uzoefu na timu ikiwa ndio mara ya kwanza inashiriki michuano hiyo.

Aidha Farid alisema, wachezaji wengi waliounda kikosi hicho walikuwa wanakabiliwa na majeraha ya mara


kia hatua ya Robo fainali ya mashindano ya Mei Mosi 2025.

# wa kwa kutinga Robo Fainali May Mosi

kwa mara, jambo ambalo lilichangia kushindwa kufikia malengo.

Naye kocha wa kikosi hicho, Abdul-shakur Abeid Abdulla, aliushukuru uongozi wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu kutokana na mashirikiano makubwa waliyoipatia timu hiyo kuanzia mwanzo hadi mwisho wa mashindano huku akiiomba Afisi iendelee kutoa msaada zaidi mwakani ili kuchukua ubingwa wa mashindano hayo.

Akizungumzia changamoto za michuano hiyo Kocha huyo alisema, wachezaji wake wengi kwenye mechi ya robo fainali ambapo walichuana na Wakala wa Bohari Kuu ya Dawa na kupoteza mchezo huo, walibanwa na majukumu ya kiafisi na wengine walikuwa na majeraha.

"Nadhani tunahitaji sapoti kubwa kutoka afisini, kama tulivyoona timu za wenzetu walivyojipanga", amesema kocha huyo.

Katika mchezo wa awali Timu ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu iliitundika goli nne kwa moja 4 -1 timu ya Wizara ya Afya katika mchezo uliofanyika Kiwanja cha Chuo cha Afya, Mbweni, Zanzibar.

Mchezo miwili ya hatua ya makundi, Timu hiyo ilitoka sare ya moja kwa moja 1-1 na Timu ya Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) pamoja na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (ZAA) .

AGC ZANZIBAR | ATTORNEY-GENERAL'S CHAMBERS

## Attorney General's Chambers

# "HAKI NA WAJIBU"



SCAN ME

Fuatilia kurasa zetu za mitandaoya kijamii.

Afisi_ya_mwanasheriamkuu_znz